TANGAZO LA SERIKALI Na. 224 La tarehe 15/4/2022

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA 290)

# SHERIA NDOGO

(*Imetungwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1)*)

SHERIA NDOGO ZA ADA NA USHURU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO ZA MWAKA 2022

Jina

1. Sheria Ndogo hizi itajulikana kama Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo ya Mwaka 2022.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"afisa mwadhiniwa" maana yake ni mtumishi wa umma yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia Sheria Ndogo hiz;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"madini ya ujenzi" maana yake ni kifusi, udongo, mchanga, tarazo, moramu, mawe, kokoto, mawe, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa

katika eneo la Halmashauri;

"wakala" maana yake ni kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Utozaji wa ada na ushuru

3.-(1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi zitalipwa kwa Halmashauri.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

4. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi.

Muda wa kukusanya ada na ushuru

5.-(1) Muda wa kukusanya ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(3) Malipo ya ada na ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Usimamizi wa Sheria Ndogo

6.-(1) Halmashauri inaweza kufunga biashara au kusimamisha uendeshaji wa shughuli yoyote ambayo itafanyika bila ya kuwa na leseni au kibali kinachotolewa na Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala wake anaweza kukamata na kuzuia mali au bidhaa za mtu yeyote ambaye ameshindwa kulipa ushuru.

(3) Endapo mmiliki wa mali au bidhaa iliyokamatwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) atashindwa kulipa ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri, baada ya kupata amri ya nahakama, itauza mali au bidhaa na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mali au bidhaa hizo baada ya kutoa ada au ushuru unaodaiwa, gharama za kuhifadhi mali au bidhaa, gharama za mahakama na gharama za mnada.

(4) Wakala hataruhusiwa kukamata mali au bidhaa bila kupata idhini ya maandishi ya Mkurugenzi.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu wa bidhaa au mali iliyokamatwa chini ya kifungu hiki isipokuwa tu kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa na Halmashauri au wakala.

Uteuzi wa wakala

7.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua wakala kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hizi;

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya afisa mwidhiniwa

8. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kwa nia ya kukusanya ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Makosa na adhabu

9.-(1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atashindwa kulipa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;
(c) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii; au
(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri shughuli zinazohitaji kulipiwa ushuru.

(2) Mtu atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1), atatoa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne.

Kufililisha kosa

10. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa TANGAZO LA SERIKALI NA. 49 la 2009 50 la2009 51 la 2009 92 la 2012

11. Sheria Ndogo zifuatazo zimefutwa:
(a) Sheria Ndogo za Kituo cha Mabasi za Halmashauri ya Wilaya ya. Kilolo, 2009. Sheria Ndogo za Masoko za Halmashauri ya Wilaya Kilolo, 2009;
(b) Sheria Ndogo za Matangazo ya Biashara za Halmashauri ya Wilaya Kilolo, 2009;
(c) Sheria Ndogo za ushuru wa Maegesho za

166 la 2012 Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, 2012;

167 la 2012
168 la 2012 (d) Sheria Ndogo za Ada za Burudani za Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, 2012;

169 la 2012 (e) Sheria Ndogo za Kodi za Huduma ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, 2012;

91 la 2015 (f) Sheria Ndogo za Vibali vya Ujenzi za Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, 2012;

(g) Sheria Ndogo za Ushuru wa Mazao Mchanganyiko za Halamashauri ya Wilaya ya Kilolo, 2012; na

(h) Sheria Ndogo za Ushuru wa Madini za Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, 2015.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 3)*

SEHEMU A.

USHURU WA MAZAO YA KILIMO NA BIASHARA

| | |
|---|---|
| 1. Mazao ya Kilimo | Asilimia 3 ya bei ya kununulia |
| 2. Mazao ya Biashara | Asilimia 3 ya bei ya kunulia |

SEHEMU B

USHURU WA MAZAO YA MIFUGO

| NA | AINA YA ZAO | USHURU (TSHS) | KIPIMO |
|---|---|---|---|
| 1 | Ngozi ya Ng'ombe | 20,000/= | Kwa ngozi 100 |
| 2 | Ngozi ya Mbuzi | 12,000/= | Kwa ngozi 100 |
| 3 | Ngozi ya Kondoo | 12,000/= | Kwa ngozi 100 |
| 4 | Tenga la Kuku | 1,000/= | Kwa kila tenga la kuku kumi (10) |
| 5 | Ushuru wa Kuwamba ngozi katika mabanda ya ngozi | 200/= | Kwa ngozi moja |
| 6 | Ushuru wa minada | 4,000/=<br>1,000/=<br>1,000/= | Ng'ombe mmoja<br>Mbuzi/Kondoo mmoja<br>Nguruwe mmoja |
| 7 | Ushuru wa ukaguzi wa nyama | 2,000/=<br>500/=<br>1,000/= | Ng'ombe mmoja<br>Mbuzi/Kondoo mmoja<br>Nguruwe mmoja |

SEHEMU C.

ADA YA KUKODI UKUMBI NA MALI ZA HALMASHAURI.

(a) Ukumbi wa Halmashauri……………………………… 100,000/= kwa siku moja.

SEHEMU D.

USHURU WA HUDUMA ZINAZOTOLEWA KATIKA HALMASHAURI

(a) Huduma zinazotolewa na Wazabuni, Kandarasi, Kampuni/tawi la Kampuni, Duka na watu binafsi wanaofanya biashara katika eneo la Halmashauri watalipa 0.3% ya mapato kwa mwezi.

(b) Wafanyabiashara wadogo ambao hawafungi hesabu watalipa Tshs 20,000 kwa mwaka kama kodi ya huduma.

SEHEMU E

Kodi ya pango WA VIBANDA VYA BIASHARA

a) kuzunguka soko la Halmashauri……………………30,000 kwa mwezi.

b) Kuzunguka vituo vya mabasi……………………………. 30,000 kwa mwezi.

c) Pango la meza katika soko la Halmashauri…………………10,000 kwa mwezi.

*Tangazo la Serikali Na. 224 (Linaendelea.)*

d) Ushuru wa kizimba/meza………………………………………. 1,000 kwa kila siku ya gulio.

SEHEMU F

USHURU WA MAEGESHO YA MAGARI KWENYE MAENEO YANAYOMILIKIWA NA HALMASHAURI

a) Magari makubwa ………….………………………….………. 3,000/= kwa siku
b) Magari madogo chini ya tani 2.5 …… …….1000 Kwa siku
c) Pikipiki…………………………………………………..………….…. 500 kwa siku
d) Pikipiki ya magurudumu matatu na Bajaji…………… 500 kwa siku

SEHEMU G

USHURU WA KULAZA MAGARI KWENYE MAENEO YANAYOMILIKIWA NA HALMASHAURI

a) Magari makubwa…………………………………………….………3,000/= kwa usiku mmoja
b) Basi la abiria zaidi ya 28 ……………………………….………. 3,000/= kwa usiku mmoja
c) Basi la abiria chini ya 28 ………………………………………. 2,000/= Kwa usiku mmoja
d) Taksi na magari mengine madogo ya watu binafsi ………. 1,000 Kwa usiku mmoja
e) Pikipiki…………………………………………….……………. 500 kwa usiku mmoja
f) Pikipiki ya magurudumu matatu na Bajaji…………… 500 kwa usiku mmoja

SEHEMU H

USHURU WA KITUO CHA MABASI

a) Basi la abiria zaidi ya 40 (basi kubwa) ……………………………………. 1,000/=
b) Basi la abiria ya zaidi ya 20 chini ya 40 (coaster)……………………. 1,000/=
c) Basi la abiria chini ya 20 (Hiace) ……………………………………………. 500/=
d) Magari madogo kama Taksi, Noah na mengine …………………………………. 500/=

SEHEMUI

USHURU WA MADINI YA UJENZI

| NA | AINA YA MADINI | KIASI (Tshs) | KIPIMO |
|---|---|---|---|
| 1 | Mawe kwa ajili ya kutengenezea chokaa | 12,000/=<br>18,000/=<br>30,000/= | Mita za Ujazo (Cubic Meter) 1 hadi 4<br>Mita za Ujazo (Cubic Meter) 4 hadi 8<br>Mita za Ujazo (Cubic Meter) 8 hadi 15 |
| 2 | Kokoto | 4,000/=<br>6,000/=<br>10,000/= | Mita za Ujazo (Cubic Meter) 1 hadi 4<br>Mita za Ujazo (Cubic Meter) 4 hadi 8<br>Mita za Ujazo (Cubic Meter) 8 hadi 15 |
| 3 | Udongo (Kifusi) | 2,000/=<br>4,000/=<br>7,000/= | Mita za Ujazo (Cubic Meter) 1 hadi 4<br>Mita za Ujazo (Cubic Meter) 4 hadi 8<br>Mita za Ujazo (Cubic Meter) 8 hadi 15 |
| 4. | Mawe kwa ajili ya ujenzi | 2,000/=<br>4,000/=<br>7,000/= | Mita za Ujazo (Cubic Meter) 1 hadi 4<br>Mita za Ujazo (Cubic Meter) 4 hadi 8<br>Mita za Ujazo (Cubic Meter) 8 hadi 15 |
| 5 | Mchanga | 2,000/=<br>4,000/=<br>7,000/= | Mita za Ujazo (Cubic Meter) 1 hadi 4<br>Mita za Ujazo (Cubic Meter) 4 hadi 8<br>Mita za Ujazo (Cubic Meter) 8 hadi 15 |

*Tangazo la Serikali Na. 224 (Linaendelea.)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6 | Chokaa | 12,000/=<br>18,000/=<br>30,000/= | Mita za Ujazo (Cubic Meter) 1 hadi 4<br>Mita za Ujazo (Cubic Meter) 4 hadi 8<br>Mita za Ujazo (Cubic Meter) 8 hadi 15 |
| 7 | Changarawe | 2,000/=<br>4,000/=<br>7,000/= | Mita za Ujazo (Cubic Meter) 1 hadi 4<br>Mita za Ujazo (Cubic Meter) 4 hadi 8<br>Mita za Ujazo (Cubic Meter) 8 hadi 15 |
| 8 | Tofali | 3,000/=<br>4,500/=<br>7,500/= | Mita za Ujazo (Cubic Meter) 1 hadi 4<br>Mita za Ujazo (Cubic Meter) 4 hadi 8<br>Mita za Ujazo (Cubic Meter) 8 hadi 15 |

## SEHEMU J
## ADA YA VIBALI VYA UJENZI

(a) Ghorofa Moja ……………………………………………………….. 120,000/=
(b) Ghorofa mbili na zaidi…………………………………………….. 150,000/=
(c) Kituo cha mafuta (Sheli)………………………………………… 250,000/=
(d) Maghala na bohari…………………………………………..………… 200,000/=
(e) Mnara wa simu ……………………………………..…………….. 300,000/=
(f) Nyumba ya Makazi na Biashara……………………………………. 40,000/=
(g) Nyumba ya Biashara (Guest House, Hotels, Shopping malls)… 50,000/=
(h) Nyumba za makazi ………………………………………………. 30,000/=
(i) Kibali ya kukata barabara …………………………………………… 50,000/=
(j) Kujenga fensi ………………………………………………………… 30,000/=
(k) Nyumba ya ibada…………………………………………………..50,000/

## SEHEMU K
## ADA YA MAOMBI YA MABADILIKO YA MATUMIZI YA JENGO LILILOPO

(a) Nyumba ya Makazi …………………………………………………. 10,000/=
(b) Nyumba ya biashara ………………………………………………… 50,000/=
(c) Ghorofa zote ……………………………………………………………….100,000/=
(d) Kiwanda, Bohari, ghara n.k ……………………………..…… 100,000/=
(e) Kituo cha Mafuta (Sheli) ……………………………………………100,000/=

## SEHEMU L

## ADA YA SHUGHULI ZA UTAMADUNI

a) Kusajili kikundi cha sanaa, ngoma, muziki Tshs. 50,000/= Kwa Mwaka

b) Kibali cha kupiga disco kwa siku moja:-
   (i) Kikundi cha ndani ya Wilaya Tshs. 20,000/=
   (ii) Kikundi cha nje ya Wilaya lakini ndani ya Mkoa Tshs. 30,000/=
   (iii) Kikundi cha nje ya Mkoa Tshs. 40,000/=

c) Kibali cha kupiga dansi kwa siku moja:-
   (i) Kikundi cha ndani ya Wilaya Tshs. 15,000/=
   (ii) Kikundi cha nje ya Wilaya lakini ndani ya Mkoa Tshs. 20,000/=
   Kikundi cha nje ya Mkoa Tshs. 30,000/=

d) Kibali cha kutengeneza vifaa vya kiutamaduni kama vinyago, vikapu, machanuo, nyungo, ngoma, michoro na maandishi Tshs. 5,000/= ambacho kitatumika kwa mwezi mmoja tu.
e) Kibali cha Sherehe Tshs. 30,000/= kwa siku.
f) Kibali cha Matangazo ya biashara kwa kutumia vipaza Sauti Tshs. 30,000/= kwa siku

*Tangazo la Serikali Na. 224 (Linaendelea.)*

g) Kibali cha kuendesha ghughuli zote za utamaduni ambazo hazijatajwa hapo juu Tshs. 10,000/= kwa siku.

h) Kibali cha kuendesha utafiti wa mambo ya kale na tafiti zingine zifananazo na hizo ni:-
   1. Raia wa Tanzania ………………….Tshs. 1,000/= kwa siku
   2. Asie Raia wa Tanzania …………US $ 5 kwa siku

*Tangazo la Serikali Na. 224 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA PILI

*(Limengenezwa chini ya kifungu cha 10)*

KUFIL ILISHA KOSA

Mimi…………………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, kwamba mnamo tarehe ………mwezi………. Mwaka………. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha………………. cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo za mwaka 2022.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halamashauri ya Wilaya ya Kilolo, Niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninayodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI KWELI NA NINAYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU
Leo tarehe………………………………. ya Mwezi…………………. Mwaka…………………
Jina…………………………………………Saini………………………………………
Mbele ya:
Jina………………………………………...Cheo…………………………………….
Saini……………………………………Tarehe……………………………………

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi za (Usafi wa Mazingira) kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 11/8/2021 mbele ya:-

LAIN E. KAMENDU,
*Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya,*
*Kilolo.*

ANNA M. MSOLA,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Kilolo.*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
2 Machi, 2022

INNOCENT L. BASHUNGWA (MB.),
*Waziri wa Nchi OR-Tamisemi,*